JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA UTAMADUNI 1997

WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI

# SERA YA UTAMADUNI 1997

WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI

## DIBAJI

Umoja, utulivu na mshikamano ambavyo Watanzania tunajivunia vimetokana na utamaduni tuliojijengea. Nguzo za utamaduni huu ni pamoja na mila na desturi zetu, lugha ya Kiswahili, sanaa na michezo, utunzaji wa mazingira, vielelezo vya utamaduni na historia yetu. Hata hivyo, bado utamaduni ulikuwa hauzingatiwi kikamilifu katika mipango yetu ya maendeleo. Nafurahi kwamba Sera hii inatoa upeo na kuanzisha mfumo ambao utaliwezesha Taifa letu kuenzi na kuimarisha utambulisho wake na kujenga **utamaduni huru** na siyo **utamadum huria**. Ufanisi katika utekelezaji wa sera hii utategemea sana ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi, mashirika, makampuni na wananchi kwa jumla. Sera hii inazingatia maoni na mapendekezo kutoka Wizara mbalimbali, mashirika ya umma na ya watu binafsi, viongozi wa dini na wataalam wa fani mbalimbali za utamaduni.

Ni matarajio yangu kwamba wananchi watapata fursa ya kuisoma na kuielewa sera hii ili waweze kushiriki kikamilifu katika uimarishaji wa utambulisho wa Watanzania.

Alhaji Profesa Juma A. Kapuya

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI**

**1997**

## YALIYOMO

**DIBAJI** 1

**SURA YA KWANZA**

**1. UTANGULIZI** 5

1.1 Dhana ya Utamaduni

1.2 Mila na Desturi

1.3 Utamaduni Kabla ya Kupata Uhuru Mwaka1961

1.4 Sekta ya Utamaduni katika Mfumo wa Serikali

1.5 Haja ya kuwa na Sera.

**SURA YA PILI**

**2. DHIMA NA MALENGO YA UTAMADUNI** 9

2.1 Dhana ya Utamaduni

2.2 Malengo ya Utamaduni

**SURA YA TATU**

**3. LUGHA** 13

3.1 Lugha ya Taifa

3.2 Lugha ya Jamii

3.3 Lugha za Kigeni

3.4 Lugha ya kufundishia

**SURA YA NNE**

**4. SANAA NA UFUNDI** **16**

4.1 Aina za Sanaa

**SURA YA TANO**

**5. UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA URITHI WETU WA UTAMADUNI** **18**

5.1 Jukumu Ia Jamii

5.2 Tathmini ya Rasilimali za Utamaduni

5.3 Rasilimali za Utamaduni Zilizopo Majini

5.4 Vitabu vya Maelezo ya Wilaya na Mikoa

5.5 Utamaduni na Uhifadhi wa Mazingira

**SURA YA SITA**

**6. BURUDANI** **22**

6.1 Maana ya Burudani

**SURA YA SABA**

**7. UTAMADUNI NA USHIRIKISHWAJI UMMA** **25**

7.1 Jamii na Utamaduni

SURA YA NANE

**8. MALEZI, ELIMU NA MAFUNZO** 27

8.1 Malezi

8.2 Elimu na Mafunzo

SURA YA TISA

**9. UENDESHAJI NA UGHARIMIAJI WA SHUGHULI ZA UTAMADUNI** 31

9.1 Uendeshaji

9.2 Maadili ya Utambulisho wa Taifa

9.3 Hakimiliki

9.4 Maendeleo ya Wananchi na Utamaduni

9.5 Ugharimiaji

9.6 Mgawanyo wa Majukumu

## SURA YA KWANZA

### 1. UTANGULIZI

#### 1.1 Dhana ya Utamaduni

Utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Kwa maneno mengine, utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine. Utamaduni ndicho kitambulisho kikuu cha taifa na ni kielelezo cha utashi na uhai wa watu wake. Kwa hiyo, umoja, utulivu na mshikamano ambavyo Watanzania tunajivunia vinatokana na utamaduni tuliojijengea. Nguzo za utamaduni huu ni pamoja na mila na desturi, lugha, sanaa, michezo na historia yetu.

#### 1.2 Mila na Desturi

Mila na desturi ni nguzo muhimu sana katika utamaduni wa jamii yoyote ile. Mila huhalalisha matendo na taratibu za jamii. Mtu akiwauliza watu kwa nini wanafanya jambo fulani, atajibiwa kuwa "ni mila yetu", wakiwa na maana kuwa ni halali kufànya hivyo. Kwa hiyo, mila ni sawa na sheria zisizoandikwa. Desturi huelezea namna jamii inavyoendesha mambo yake. Yaani, namna ambavyo kwa kawaida watu katika jamii hufanya mambo yao.

Mila na desturi hujengwa, hukomaa, hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na pia huweza kufifia na kupotea. Desturi huanza kama tabia ya mtu au kundi la watu. Tabia hii ikienea kwa jamii nzima hugeuka kuwa desturi. Desturi zikiota mizizi zikawa ndizo namna halali ya kufanya mambo hugeuka kuwa mila. Kwa hiyo, mila na desturi siyo mambo ya kizamani na wala siyo mambo ambayo nchi yetu inapaswa kuondokana nayo. Wakati wote mila na desturi mpya hujitokeza na nyingine hupotea. Ni mila zipi au desturi zipi zinapotea au kujitokeza na kuendelea hutegemea mtazamo na msukumo wa jamii. Jamii hukemea tabia mbaya ili zisisambae na kugeuka kuwa desturi. Aidha jamii huzisifia na kuzilinda mila na desturi nzuri.

Kadri muda unavyopita na mazingira ya kijamii kugeuka baadhi ya mila na desturi hupitwa na wakati. Linakuwa ni jukumu la jamii kuachana na mila na desturi hizo na kubuni mila na desturi mpya zinazokidhi mahitaji yake. Baadhi ya mila na desturi nzuri, katika Taifa letu ambazo zinastahi!i kuendelezwa ni:

(a) Kuenzi Utambulisho wa Taifa,

(b) Kuwa na tahadhari dhidi ya majanga,

(c) Kujenga usawa wa kujinsia.

Baadhi ya mila na desturi mbaya ambazo hazina budi kupigwa vita na kutokomezwa kabisa ni:

(a) Kutokuwepo kwa tabia ya utunzaji wa mali na rasilimali za Taifa,

(b) Uchafuzi wa mazingira,

(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya,

(d) Kutokuthamini kazi,

(e) Udhalilishaji na unyanyasaji wa wanawake na watoto.

Hatua zozote zinazosaidia kutambua na kuimarisha mila na desturi nzuri na kupiga vita mila na desturi mbaya ni muhimu katika kutimiza malengo na kuinua dhima ya utamaduni.

### 1.3 Utamaduni Kabla ya Kupata Uhuru Mwaka 1961

Kabla ya ujio wa wakoloni katikati ya karne ya kumi na tisa, jamii za Tanzania ya sasa zilikuwa na tamaduni zake zilizotofautiana kutokana na tofauti za mifumo ya kiuchumi, kijamii na mazingira. Pia, jamii hizi zilikuwa na lugha zilizobeba dhana za mitazamo na taratibu za kuendesha maisha. Aidha, jamii hizi zilijitosheleza, kujiamini na zilikuwa na taratibu zake za kujilinda dhidi va maadui na namna ya kujitibu na kujikinga dhidi ya maradhi mbalimbali. Kila mwananchi alitekeleza majukumu ya kazi kwa kujituma. Pia, jamii zilijenga taratibu za ushirikiano na mawasiliano ndani ya jamii zenyewe na baina ya jamii moja na jamii nyingine.

Ukoloni uliingiza mifumo tofauti ya kiuchumi na kijamii na tamaduni zilizokuwepo zikaanza kubadilika. Mitazamo na taratibu za kidini, mavazi, lugha na kadhalika viligeuzwa kwa njia ya kwenda sambamba na tamaduni za kigeni. Isitoshe, wakoloni walijaribu sana kuwafanya wananchi waamini kwamba hawakuwa na utamaduni au kwamba utamaduni wao haukufaa, na kuwa walitakiwa wauonee haya. Badala yake walilazimishwa kuchukua utamaduni wa wageni waliotawala na kumiliki uchumi. Hata hivyo, wakoloni hao hawakufaulu kufuta kabisa tamaduni za asili kama walivyodhamiria.

**1.4 Sekta ya Utamaduni Katika Mfumo wa Serikali**

Tulipopata Uhuru mwaka 1961, Serikali ilianza jitihada za kujenga Taifa ambamo watu wake wangejumuishwa kuwa kitu kimoja. Kwa kutambua umuhimu wa utamaduni katika jitihada hizi, Serikali, kwa mara ya kwanza, iliunda **Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana** kusimamia masuala ya utamaduni mwaka 1962. Baada ya hapo utamaduni uliendelea kushughulikiwa chini ya Wizara mbalimbali kama ifuatavyo:

- 1962 - Wizara ya Utamaduni wa Taifa Vijana.
- 1964 - Ofisi ya Rais.
- 1967 - Wizara ya Tawala za Mikoa na Maendeleo Vijijini.
- 1968 - Wizara ya Elimu ya Taifa;
- 1974 - Wizara ya Utamaduni wa Taifa naVijana;
- 1980 - Wizara ya Habari na Utamaduni;
- 1984 - Ofisi ya Waziri Mkuu;
- 1985 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo.
- 1988 - Wizara ya Kazi, Utamaduni na Ustawi wa Jamii.
- 1990 - Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Katika kipindi chote hiki, jitihada kubwa za kuendeleza utamaduni wetu zimefanyika, kama vile:

(a) Kuwasaidia wasanii kuunda vikundi au vyama vyao;

(b) Kuzipa msukumo sanaa;

(c) Kutukuza na kuhimiza matumizi ya lugha yetu ya Taifa, Kiswahili;

(d) Kutumia sanaa kukemea mila na desturi zisizokubalika na kuenzi mila na desturi nzuri;

(e) Kuuhimiza umma kutambua umuhimu wa kuhifadhi kumbukumbu na historia ya nchi yetu;

(f) Kuyapatia msukumo maendeleo ya nchi yetu kimichezo.

Lakini, pamoja na mafanikio makubwa yaliyotokana na jitihada hizi za Serikali, bado zilikuwepo kasoro kubwa mbili ambazo ni kutokuwepo kwa Sera ya Utamaduni na kuhamishwa mara kwa mara kwa Sekta ya Utamaduni kutoka Wizara moja hadi nyingine kama ilivyoelezewa hapo juu. Jitihada zote za kuendeleza utamaduni zilikuwa hazifanikiwi ipasavyo kutokana na ukosefu wa dira na kutokuwepo kwa uhakika wa Sekta yenyewe kuwepo katika Wizara moja kwa muda mrefu.

**1.5 Haja ya kuwa na Sera**

Ukosefu wa Sera ya Utamaduni husababisha jamii kutojiamini na kukosa mwelekeo. Utambulisho wa Taifa ni lazima uwe ndiyo kiini na dira ya maendeleo. Serikali imeona haja ya kuwa na Sera ya Utamaduni ambayo itatoa mwelekeo wa maendeleo ya Utamaduni na kuweka wazi majukumu ya Serikali, wananchi na vyombo mbalimbali vya umma na watu binafsi. Sera hii italiwezesha Taifa kutumia kikamilifu fani zote za utamaduni katika kujenga na kutathmini maendeleo na maisha ya Mtanzania. Lengo la Sera hii ni kuelezea dhima na malengo ya utamaduni; kuainisha jinsi shughuli za utamaduni zitakavyoendeshwa na kusimamiwa, kuelezea nafasi ya lugha za kijamii, lugha ya Taifa, ambayo ni Kiswahili, na lugha za kigeni katika Taifa; kusisitiza umuhimu wa kuhifadhi na kuendeleza urithi wetu wa utamaduni, ikiwa ni pamoja na burudani, michezo, malezi, elimu na mafunzo, kufafanua jinsi umma utakavyoshirikishwa katika shughuli za utamaduni; na kuweka taratibu mpya za kugharamia uendeshaji wa shughuli za utamaduni.

## 2. DHIMA NA MALENGO YA UTAMADUNI

Ingawa Sekta ya Utamaduni imekuwa katika Mfumo wa Serikali tangu mwaka 1962, nafasi yake katika maendeleo ya Taifa bado haijatambuliwa kikamilifu. Mipango ya maendeleo imekuwa ikibuniwa na kutekelezwa bila kujali utamaduni wa wananchi. Kwa mfano, matumizi ya uzoefu, stadi na elimu ya jadi havitiliwi maanani. Utamaduni haupewi dhima katika maamuzi na mipango ya maendeleo kwa sababu inaaminika kuwa maendeleo ni kuondokana na mambo ya kiasili pasipo kuchunguza misingi ya mambo hayo na faida zake. Yote haya yametokana na kutokueleweka kwa dhana ya utamaduni.

### 2.1 Dhima ya Utamaduni

#### 2.1.1 Utamaduni na Maendeleo

Utambulisho madhubuti wa utamaduni ni muhimu katika kujenga na kuendeleza moyo wa kujiamini katika maendeleo ya jamii yoyote ile. Utambulisho huu umo katika vielelezo vya utamaduni ambavyo vina mguso wa kipekee ambao unakamilika pale unaposababisha kuwepo kwa hisia na taasisi za udhihirisho wa jamii hiyo. Uthibiti huo unasimikwa katika hisia na taasisi za jamii zinazohusika.. Maendeleo halisi hayawezi kupatikana bila kuzingatia hisia na taasisi za aina hii. Kupuuzwa kwa ukweli huu katika mipango ya maendeleo husababisha kutofanikiwa kwa mipango hiyo.

#### 2.1.2 Utamaduni na Teknolojia

Utamaduni ni matokeo ya uhusiano baina ya binadamu na mazingira yake. Mbinu mojawapo ambayo binadamu anatumia katika mahusiano haya ni teknolojia yaani ubunifu wa vifaa an zana, stadi, mbinu na taratibu za kufikiri na kutenda iii kudumisha uhai na kuboresha hail ya maisha ya binadamu na mazingira yake. Hivi sasa Tanzania inatumia teknolojia za ama mbili teknolojia ya na teknolojia ya kisasa. Teknolojia hizi mbili zmatümika sambamba, zinaingiliana na ingefaa zote ziendelezwe.

### 2.1.3 Utambulisho wa Taifa

Nchi yoyote ile huru lazima ijivunie utamaduni wake na iwe na itikadi na vitu vya kuitambulisha kama vile lugha, bendera ya taifa, wimbo wa taifa, vazi la taifa na kadhalika. Vitambulisho vya ama hii ndivyo vinavyo liwezesha taifa kujenga umoja na mshikamano. Baadhi ya tabia na vitu ambavyo Watanzania wanajivunia kuwa ni kielelezo cha uhuru na utaifa wao ni:

- Bendera ya Taifa;
- Nembo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano;
- Wimbo wa Taifa;
- Kuthamini na kuheshimu kazi; Kujitegemea,
- Umoja, amani na utulivu;
- Kuheshimu na kuthamini utu na uhuru wa mtu;
- Lugha ya Kiswahili;
- Mbio za Mwenge;
- Maumbile asilia kama vile, Mlima Kilimanjaro,
- Kreta ya Ngorongoro na Mbuga za Serengeti;
- Twiga.

### 2.1.4 Utamaduni na Elimu

Elimu ni ujuzi na uzoefu ambao jamii, kupitia utamaduni wao, wamejipatia na wanaurithisha kwa jarnii na vizazi vijavyo kwa lengo Ia kukidhi mahitaji ya jamii hiyo.Hivyo, elimu haipaswi kutenganishwa na utamaduni. Kwa mantiki hii, elimu inatakiwa iimarishe utambulisho wa taifa kwa kurithisha na kuneemesha mila, desturi nzuri na maadili.

## 2.2 Malengo ya Utamaduni

Malengo ya Utamaduni ni:

### 2.2.1 Kujenga na Kudumisha Utambulisho wa Jamii kwa:

(a) Kuitambulisha jamii;

(b) Kurithisha na kuendeleza, historia, mila na desturi;

(c) Kuwa na lugha karna chombo cha mawasiliano na kurithisha utamaduni,

(d) Kujenga utu, rnoyo wa kujiarnini na kuheshimu utu na watu wengine;

(e) Kujenga tabia ya kutarnbua na kuheshimu haki binafsi na za watu wengine.

### 2.2.2 Kujenga na Kuhimiza Maendeleo ya Jamii kwa:

(a) Kutarnbua na kulinda rasilimali. mazmgira na urithi wa utarnaduni;

(b) Kuhakikisha na kuhirniza usawa katika rnatumizi bora na mgawanyo wa haki wa rasilimali na miliki;

(c) Kuenzi na kutunza tabia njema na kukemea vitendo viovu kama vile rnatumizi ya madawa ya kulevya, ubakaji, ulevi. Uvivu, uzembe, uzururaji na umalaya;

(d) Kutarnbua na kuthamini kazi halali kuwa ni rnsingi wa maisha na rnaendeleo ya binadamu;

(e) Kuiandaa jarnii kutambua kwamba elimu, mafunzo na ubunifu ni muhimu katika kuzalisha mali na kuendesha mambo, ili kuongeza tija na kuleta ufanisi;

(f) Kutharnini na kutumia ujuzi, taaluma na teknolojia ya jadi katika kuimarisha afya, matumizi bora ya mazingira, rasilimali na kuendeleza jamii;

(g) Kuinua hali ya maisha ya jamii.

### 2.2.3 Kurithisha na Kuendeleza Maadili, Mila na Desturi Nzuri kwa:

(a) Kuhimiza utunzaji wa mali na rasilimali za taifa;

(b) Kupiga vita ubaguzi na udhalilishaji wa kijinsia;

(c) Kuhimiza tabia ya kuheshimu utu, watu na sheria;

(d) Kujenga tabia ya usafi, uhifadhi na matumizi bora ya rasilimali na mazingira;

(e) Kujenga tabia ya kutambua, kuenzi na kuheshimu vitambulisho vya taifa;

(f) Kujenga tabia ya kujiandaa na kuchukua tahadhari dhidi ya majanga;

(g) Kujenga taifa lenye nidhamu.

#### 2.2.4 Kukuza na Kuendeleza Uhusiano kwa:

(a) Kujenga tabia ya ushirikiano, mshikamano, udugu, uzalendo, upendo na moyo wa kuvumiliana;

(b) Kulitambulisha na kulitangaza taifa nje ya mipaka yake na kuimarisha uhusiano wa kimataifa.

#### 2.2.5 Ushirikishwaji Umma kwa:

(a) Kuweka taratibu za kuiburudisha na kuineemesha jamii kiakili na kimwili;

(b) Kuweka taratibu bora za utawala na uongozi katika jamii, taratibu ambazo zinajenga mshikamano bila kujali tofauti za imani, dini, jinsia, umri wala rangi;

(c) Kuushirikisha umma katika masuala yote yanayohusu uhai wa jarnii na utarnaduni wao.

Malengo haya ya utamaduni, kwa parnoja, yanaonyesha kuwa dhima ya utamaduni ni kubwa sana. Ndiyo maana Umoja wa Mataifa umekuwa ukihimiza nchi zote wanachama kutoa kipaumbele na kuzingatia utamaduni katika shughuli zote za maendeleo. Muongo wa Dunia wa Maendeleo ya Utamaduni (World Decade for Cultural Development) mwaka 1987 hadi 1997, ulibuniwa kwa ajili hiyo. Hivyo, Tanzania haina budi kuendelea kuuenzi utamaduni wake.

## 3. LUGHA

Tanzania ina jamii zaidi ya mia na kila moja ya jamii hizi ina lugha yake. Lakini, kutokana na jiografia na aina mbalimbali za mawasiliano kama vile biashara, kuna jamii ambazo lugha zao zinakaribiana kimaumbile na kwa maneno na hivyo kuziwezesha jamii hizi kusikilizana. Nchi yetu ma lugha za aina tatu: lugha za jamii, lugha ya Taifa yaani Kiswahili na lugha za kigeni, kwa mfano, Kiingereza na Kifaransa. Aidha, kutokana na mahusiano na mawasiliano ya muda mrefu, Kiswahili, pamoja na lugha nyingine za jamii zimetohoa, kujumuisha na kubadilisha baadhi ya maneno ya lugha za kigeni, kama vile Kireno, Kiarabu, Kijerumani, Kiingereza na Kifaransa kuwa ya Kiswahili.

### 3.1 Lugha ya Taifa

Kiswahili ndiyo lugha pekee ambayo huzungumzwa na kueleweka na watu wengi katika nchi nzima. Tangu wakati wa kuanzishwa na kuenezwa kwa utawala wa kikoloni katika karne ya kumi na tisa hadi baada ya kupata Uhuru mwaka 1961, Kiswahili kimeendelea kutumika kama Lugha ya Taifa. Ingawa tangu tulipopata Uhuru kumekuwa na matamshi mbalirnbali ya kisiasa na maagizo ya kiserikali kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Taifa, bado Kiswahili hakijatamkwa kisheria kuwa ni Lugha Rasmi ya Taifa. Ukosefu wa tamko rasmi kuhusu nafasi ya Kiswahili katika taifa letu unasababisha, pamoja na mambo mengine:

- Wananchi kukosa haki kwani sheria zetu zimeandikwa kwa lugha ya Kigeni. Aidha, shughuli za mahakama za ngazi za juu huendeshwa kwa lugha ya Kigeni;
- Kuwepo kwa mkanganyiko katika mawasiliano rasmi ya Kiserikali.

Pamoja na ukeli kwamba lugha ndiyo kitambulisho kikuu cha taifa lolote lile, na kwamba Tanzania imeweza kujenga na kukuza umoja wa kitaifa kutokana na matumizi ya lugha ya Kiswahili, bado kumekuwepo na hisia kwamba matumizi ya lugha ya Kiswahili yataifanya Tanzania isiwe na maendeleo ya kisayansi na teknolojia ya kisasa. Lakini inatambulika duniani kote kwamba, hakuna nchi yo yote ile ambayo imekuwa na maendeleo ya kuridhisha ya kisayansi na kiteknolojia bila ya kutumia lugha yake ya taifa. Kwa hiyo:

**3.1.1. Kiswahili kitatamkwa rasmi kuwa Lugha ya Taifa na kauli hii itazingatiwa katika Katiba ya Nchi.**

**3.1.2. Vitawekwa vivutio kwa watu binafsi na Mashirika mbalimbali kuchapisha na kusambaza maandiko katika lugha ya Kiswahili.**

**3.1.3. Baraza Ia Kiswahili Ia Taifa litakuwa na Jukumu la kutafiti, kuneemesha na kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili.**

**3.1.4. Baraza la Kiswahili la Taifa na Taasisi nyingine za ukuzaji wa Kiswahili zitaimarishwa na kupatiwa nyenzo na fursa ya kutekeleza majukumu yake kikamilifu.**

**3.1.5. Lugha za asili zitaendelea kutumika kama hazina na chanzo cha kukuza Kiswahili.**

### 3.2 Lugha za Jamii

Lugha za jamii ni hazina kuu ya historia, mila, desturi, teknolojia na utamaduni wetu kwa jumla. Aidha, lugha hizi ni msingi wa lugha yetu ya taifa, yaani Kiswahili. Kwa hiyo:

**3.2.1. Jamii zetu zitaendelea kutumia na kujivunia lugha zake za asili.**

**3.2.2. Wananchi, mashirika ya umma na va watu binafsi yatahamasishwa kuandika, kukusanya, kutafiti, kuhifadhi na kutafsiri lugha za asili katika lugha nyinginezo.**

**3.2.3. Uandishi wa kamusi na vitabu vya sarufi za lugha za asili utahimizwa.**

**3.2.4. Mashirika ya umma na ya watu binafsi, yatahimizwa kuchapisha na kusambaza maandiko katika lugha za asili.**

### 3.3 Lugha za Kigeni

Lugha za kigeni zimetuwezesha kuwasiliana na watu wa mataifa mengine na kuendesha shughuli za kibiashara. Hata baada ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia, bado Tanzania itaendelea kuwasiliana na nchi nyingine katika nyanja mbalimbali kwa kutumia lugha za kigeni. Hivvo, kuna umuhimu wa kuhimiza ufundishaji wa lugha za kigeni shuleni. Hivi sasa lugha za kigeni ambazo zinafundishwa katika Mfumo Rasmi wa Elimu ni Kiingereza na Kifaransa. Kwa hiyo:

**3.3.1. Kiingereza kitakuwa ni somo Ia lazima katika elimu ya awali, msingi na sekondari na kitahimizwa katika elimu ya juu na ufundishaji wake utaboreshwa.**

**3.3.2. Ufundishaji wa lugha za Kifaransa, Kireno, Kirusi n.k. utahimizwa.**

### 3.4 Lugha ya Kufundishia

Katika Mfumo Rasmi wa Elimu, Kiswahili kinatumika kama lugha ya kufundishia katika elimu ya awali, msingi, mafunzo ya Cheti cha Elimu ya Ualimu na elimu ya watu wazima. Kuanzia ngazi ya elimu ya sekondari hadi elimu ya juu Kiingereza ndiyo lugha ya kufundishia. Utaratibu huu umedhoofisha lugha ya Kiswahili pamoja na maendeleo ya elimu, sayansi na teknolojia nchini. Jitihada za serikali yoyote ile ya kujenga umoja na mshikamano wa kitaifa kwa kutumia Mfumo Rasmi wa Elimu ambao hautumii lugha ya taifa kama lugha ya kufundishia zinasababisha siyo tu uharibifu wa urithi wa utamaduni wa nchi hiyo, bali pia zinachangia katika kuleta na kuendeleza umaskini na mtafaruku katika jamii. Hali hii inatokana na kiwango cha chini cha wananchi walio wengi cha kuelewa, kuzungumza na kuandika lugha za kigeni zinazotumiwa kufundishia. Kama tutaendelea kufundisha kwa lugha ya Kiingereza sayansi na teknolojia ambayo tunaihitaji sana kwa maendeleo ya taifa letu katika karne ya ishirini na moja itaendelea kuwa haki ya watu wachache wanaofahamu Kiingereza. Ili Tanzania iweze kupata maendeleo katika nyanja za elimu, sayansi na teknolojia sera zifuatazo zitatekelezwa:

**3.4.1. Mpango maalumu wa kuiwezesha elimu na mafunzo katika ngazi zote kutolewa katika lugha ya Kiswahili utaandaliwa na kutekelezwa.**

**3.4.2. Somo la Kiswahili litakuwa ni somo Ia lazima katika ngazi ya elimu ya awa1i, msingi na sekondari, na Iitahimizwa katika elimu ya juu. Aidha, ufundishaji wake utaboreshwa.**

## 4. SANAA NA UFUNDI

**Sanaa ni fani muhimu ya utamaduni ambayo ni ustadi wa kuweka na kupanga fikra kwa njia ya hisia na zana.** Sanaa inaweza ikawa ni kitu, utaratibu wa kuchezesha mwili, miondoko, utoaji wa sauti, uzungumzaji au uandishi wenye mpangilio maalum ukiwa na lengo la kutoa ujumbe na kukidhi matumizi na mahitaji ya namna mbalimbali ya binadamu. Sanaa zinajumuisha tamthiliya, muziki, ngoma, dansi, sarakasi, na kazi za mikono kama vile uchoraji, uchongaji, uhunzi, usukaji. ufumaji, ushonaji na ususi. Aidha, usanifu wa majengo au maumbo mengine na mapishi ni fani ambazo huhusishwa na ubunifu unaotokana na hisia na hivyo kuzipatia sifa ya kuwa sanaa. Tangu enzi za kale sanaa huambatana na ufundi, elimu na mafunzo na huwa na lengo rnaalum la kukidhi mahitaji ya jamii.

### 4.1 Aina za Sanaa

Sanaa zimegawanyika katika sehemu kuu tatu: **Sanaa za Ufundi, Sanaa za Maonyesho na Muziki. Sanaa za Maonyesho** ni kama vile ngoma, tamthiliya, fasihi andishi na fasihi simulizi. Sanaa hizi huleta hisia, huelezea na hutoa ujumbe kwa jamii kama njia mojawapo ya kutoa. elimu, kuhimiza maendeleo na kuleta mabadiliko katika jamii. **Sanaa za Ufundi** zinahusu utengenezaji wa vitu vinavyotumika katika maisha ya kila siku kama vile vyungu, vikombe, nyungo, chuma, visu na nakshi za aina mbalimbali. **Muziki** unahusu muziki wa ala tupu, nyimbo rnbalimbali, muziki wa ngoma za jadi, brasi, dansi, disko, okestra na muziki wa taarab. Katika mfumo wa jadi Sanaa za Ufundi, Sanaa za Maonyesho na Muziki vilienda pamoja. Licha ya mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yaliyotokea hapa nchini tangu enzi za ukoloni hadi sasa, bado sanaa zetu hazijatambuliwa kuwa ni nyenzo ya kuleta maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hali hii ikiachiwa kuendelea taifa letu litapoteza nyenzo hii muhimu ya kuchochea maendeleo. Ili kurekebisha hali hii sera zifuatazo zitatekelezwa:

**4.1.1. Baraza la Sanaa la Taifa litawashirikisha na kuwaendeleza wasanii na litakusanya na kusambaza taarifa kuhusu bei na masoko ya sanaa kwa wasanii, mashirika na watu binafsi. Aidha, Baraza litawahamasisha wasanii kushiriki katika matamasha na maonyesho mbalimbali.**

4.1.2. Mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu itajumuisha masomo ya sanaa mbalimbali, kwa mfano: muziki, uchoraji, uchongaji na tamthiliya. Aidha, masomo haya yatatahiniwa katika mitihani ya mwisho ya ngazi hizi za elimu na katika shughuli zao za siku hadi siku.

4.1.3. Wasanii watahamasishwa kuanzisha vyama vyao vya aina mbalimbali vitakavyoendeleza na kutetea maslahi yao.

4.1.4. Serikali itahakikisha kunakuwepo na utaratibu wa kuwatambua na kuwaenzi wasanii maarufu wa kitaifa.

4.1.5. Wasanii watatakiwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira.

4.1.6. Wasanii watatakiwa kuuhamasisha umma kulinda na kuhifadhi mazingira.

4.1.7. Tasnia za utamaduni zitatambuliwa na zitahimizwa kutoa mchango wake katika maendeleo ya uchumi wa Taifa.

4.1.8. Asasi zinazoshughulika na utangazaji wa biashara na bidhaa za Tanzania zitahamasishwa kutambua na kutangaza bidhaa za sanaa na muziki.

4.1.9. Serikali itahakikisha kuwa panakuwepo na jengo la kisasa la maonyesho ya sanaa katika ngazi ya Taifa. Aidha, wananchi watahamasishwa kuhakikisha kwamba wanatenga maeneo ya maonyesho.

4.1.10. Serikali itaendelea kutenga na kulinda maeneo ya kuendeshea shughuli za sanaa za ufundi, maonyesho na muziki katika miji na vijiji.

4.1.11. Vitawekwa vivutio kwa watu binafsi na mashirika mbalimbali kujenga na kuendesha kumbi za maonyesho.

## 5. UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA URITHI WETU WA UTAMADUNI

Urithi wetu wa Utarnaduni ni pamoja na viumbe, uoto, maumbile asilia, mazingira, vitu na zana za mila na desturi zinazohamishika na zisizohamishika na nyaraka za aina mbalimbali za mashirika, madhehebu ya dini, Serikali na watu binafsi. Yote haya huweza kuhifadhiwa ama kimaumbile, kisimulizi au kimaandishi. Shabaha ya kuhifadhi vitu vyote hivi ni kutunza habari na taarifa zmazotuwezesha kuelewa historia ya viumbe, chimbuko la mwanadamu na maendeleo yake kimaumbile na kiutamaduni, na uhusiano wake na mazingira, viumbe vingine, mila na desturi za watu wa kale na wa sasa. Aidha, kabla ya kuwa na maandishi, mambo yote ya muhimu ya jamii yalihifadhiwa katika simulizi. Kila kizazi kilijifunza kwa njia ya mapokeo kama vile hadithi, nyimbo na methali. Kutokana na kuanza kufundishwa kwa stadi ya kuandika, uzito wa simulizi ulipungua kwa sababu kumbukumbu nyingi ziliwekwa katika rnaandishi.

### 5.1 Jukumu la Jamii

Jamii zetu zote zinafahamu na kutambua urithi wetu wa utamaduni. Siku hizi baadhi ya watu hawauthamini urithi huu. Kiserikali, jitihada za kuhifadhi urithi huu zinafanywa na Idara ya Nyaraka za Taifa, Mambo ya Kale, Shirika la Makumbusho ya Taifa na Bodi ya Huduma za Maktaba. Bado ni mikoa, wilaya, mashirika na watu binafsi wachache tu ambao wanajihusisha na kazi hii. Serikali kuu imeachiwa mzigo wa kuhifadhi, kulinda, kutafiti na kuendeleza urithi wetu wa utamaduni. Tukiendelea na mtazamo huu na kama hatua maalum hazitachukuliwa, urithi wetu utaendelea kupotea. Ni wajibu wa kila mwananchi kuhifadhi na kuendeleza urithi wake wa utamaduni. Kwa hiyo:

**5.1.1.** **Kazi ya kulinda na kuendeleza urithi wetu wa utamaduni ni jukumu la jamii nzima na itasimamiwa na Serikali.**

**5.1.2.** **Wananchi, mashirika ya umma na ya watu binafsi watahamasishwa kutambua, kuthamini, kulinda na kuendeleza urithi wetu wa utamaduni. Aidha, umuhimu wa uhusiano uliopo baina ya mila, desturi, utamaduni, maliasili, mazingira na mipango ya mandeleo utasisitizwa.**

5.1.3. Itahakikishwa kwamba vituo vya urithi wetu wa utamaduni\vinakuwa vituo vya elimu na mafunzo na pia vivutio vya watalii.

5.1.4. Mitaala yote ya elimu na mafunzo itahimiza matumizi ya vituo na maeneo ya mambo ya kale, makumbusho, maktaba, nyaraka, maumbile asilia, uoto na mazingira katika utoaji wa elimu na mafunzo nchini.

5.1.5. Zitawekwa taratibu zitakazoliwezesha taifa kutambua, kumiliki na kuhifadhi tunu za kitaifa, ikiwa ni pamoja na sanaa za aina mbalimbali, maliasili, madini na masalia ya viumbe au vifaa vya kale.

5.1.6. Maeneo yenye urithi wa utamaduni yatatambuliwa, kutengwa na kuendelezwa, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa makumbusho za vituo.

5.1.7. Serikali itahakikisha kwamba ofisi zote za umma, mashirika na watu binafsi wanatambua, kuthamini na kutunza nyaraka walizonazo na watakazoziandika ili kuhifadhi historia na utamaduni wetu.

5.1.8. Mafunzo kuhusu utunzaji wa nyaraka yatatolewa kwa viongozi na waajiriwa wapya na katika vyuo vinavyotoa mafunzo ya uhazili, utawala na uongozi.

5.1.9. Viongozi mahali pa kazi watatakiwa kuwajibika kikamilifu na utunzaji wa maandiko na nyaraka zinazotokana na utendaji wao wa kazi wa siku hadi siku.

5.1.10. Serikali itahimiza mikoa, wilaya, vijiji, mashirika ya umma na ya watu binafsi na wananchi kwa jumla kuanzisha na kuendeleza makumbusho za aina mbali mbali, maktaba na hifadhi za nyaraka.

5.1.11. Vitu vyote vilivyotengenezwa na binadamu vitatambulika, kisheria, kuwa ni kumbukumbu za taifa vinapofikisha umri wa miaka mia moja.

## 5.2 Tathmini ya Rasilimali za Utamaduni

Kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa urithi wetu wa utamaduni wakati wa kutekeleza mipango na miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile: ujenzi wa nyumba na miji, na uchimbaji wa barabara, mabwawa ya maji na madini. Uharibifu huu umetokana na ukosefu wa sera na sheria ambazo zingewataka na kuwabana watekelezaji wa miradi ya aina hii kufanya tathmini za athari za miradi hiyo kwa rasilimali za utamaduni kabla ya miradi hiyo haijateke1ezwa. Ili kudhibiti hali hii:

**5.2.1. Uendelezaji wa ardhi na miradi yote utatanguliwa na tathmini ya athari zake kwa rasilimali za utamaduni. Gharama za tathmini hizi zitakuwa ni sehemu ya gharama za miradi yenyewe.**

## 5.3 Rasilimali za Utamaduni Zilizopo Majini

Baadhi ya urithi wetu wa utamaduni kama vile mabaki ya vyombo vya baharini vilivyozama, makazi ya kale na kadhalika, upo chini ya bahari, mito na maziwa. Sheria zilizopo hivi asa hazifafanui kikamilifu miliki ya vitu hivi. Ili kurekebisha hali hii:

**5.3.1. Miliki ya rasilimali za utamaduni zilizopo majini kama vile mabaki ya meli zitatambuliwa, kufafanuliwa na kulindwa kisheria.**

## 5.4 Vitabu vya Maelezo ya Wilaya na Mikoa (District and Regional Books)

Wakati wa utawala wa kikoloni watendaji na viongozi wakuu wa Serikali katika ngazi za wilaya na mikoa walikuwa na utaratibu wa kukusanya, kuandika na kuhifadhi taarifa rnbalimbali zilizohusiana na masuala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni katika maeneo yao. Taarifa hizi zilitunzwa katika majuzuu yaliyojulikana kama Vitabu vya Wilaya na Mikoa (District and Regional Books). Baada ya nchi yetu kupata Uhuru viongozi na watendaji wa wakuu wa serikali walioshika madaraka ya kiutawala katika ngazi za wilaya na mikoa waliutelekeza utaratibu huu kwa madai kwamba ulikuwa ni sehemu ya ukoloni. Ili kuwawezesha viongozi wapya kuyafahamu maeneo yao ya kazi kwa urahisi zaidi:

**5.4.1.** **Utaratibu wa Makatibu Tawala kuandika na kutunza majuzuu ya wilaya na mikoa, ili kuweka bayana mazingira ya jamii za mikoa na wilaya zinazohusika utaanzishwa tena.**

### 5.5 Utamaduni na Uhifadhi wa Mazingira

Utamaduni ni matokeo ya uhusiano baina ya binadamu na mazingira yake. Mazingira ni pamoja na jamii inayohusika, maumbile asilia, mandhari, ardhi, uoto na wanyama ambao wamo katika maeneo yanayohusika. Katika mahusiano haya hujengeka tabia, mila na desturi zinazohusiana moja kwa moja na mazingira. Baadhi ya tabia, mila na desturi hizi husaidia kuhifadhi mazingira na nyingine husababisha uharibifu. Uharibifu wa mazingira tunaoshuhudia hivi sasa umetokana na tabia na desturi mbaya ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia zisizo sahihi. Ili kuhifadhi na kuendeleza mazingira:

**5.5.1.** **Ujuzi, stadi na teknolojia za jadi zinazolinda mazingira zitatambuliwa na matumizi yake kuhimizwa.**

**5.5.2.** **Utafiti wa mila na desturi zenye kulinda mazingira utahimizwa ili uziwezeshe mila na desturi hizo kutambuliwa na kutumika.**

**5.5.3.** **Utafiti wa mila na desturi zenye kuchochea uharibifu wa mazingira utahimizwa ili mila na desturi hizo zitambuliwe na kukomeshwa.**

**5.5.4.** **Fani mbalimbali za utamaduni zitatumiwa kuhimiza matumizi ya mila na desturi za kuhifadhi mazingira na kusambaza matokeo ya utafiti uliofanyika.**

# 6. BURUDANI

## 6.1 Maana ya Burudani

Burudani ni shughuli ambazo mtu anazifanya kwa hiari yake ili kurudisha nguvu, akili na ari alizotumia wakati wa kufanya kazi. Aidha, burudani humfariji mtu kimwili, kiakili, kiuchumi, kielimu, kijamii na ni kiungo kati ya mtu na mazingira yake. Shughuli za burudani ni pamoja na maongezi, kupunga upepo, kusoma vitabu na magazeti, kushiriki katika michezo na sanaa za aina mbalimbali, kutalii, kuangalia televisheni, kusikiliza redio na kadhalika. Michezo kama sehemu ya utamaduni, huwaunganisha watu kwa hiari na ni muhimu katika malezi na maisha ya kila siku ya binadamu. Mtu anayeshiriki katika michezo hujenga fikra, utii, nidhamu na moyo wa kujiamini. Burudani pia hutumika katika kutoa elimu kwa jamii, kujenga udugu na mahusiano baina ya wananchi na nchi mbalimbali. Aidha, burudani ni nyenzo ya kuhimiza na kuimarisha utendaji kazi.

Taifa linatambua kwamba kila mtu anayefanya kazi zake kikamilifu anastahili kupumzika ili aweze kupata ari na nguvu mpya ya kufanya kazi zake vizuri zaidi baadaye. Hivi karibuni dhana hii imeanza kupotoshwa kwa kuzigeuza burudani na michezo kuwa ni anasa zisizokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na shughuli za uzalishaji mali katika jamii. Isitoshe, huko vijijini sehemu na aina za burudani ni chache na kuna upungufu mkubwa wa vifaa na nyenzo. Aidha, hakuna utaratibu maalum wa kuendesha na kudhibiti hata hizo sehemu na burudani chache zilizopo. Kwa ujumla wake, kuna umuhimu wa kurejesha dhana ya asili ya burudani na kudhibiti utoaji na upatikanaji wake. Aina na taratibu za michezo na burudani ziwe ili zile zinazoimarisha maadili, kuongeza ufanisi wa kazi, elimu, kipato cha wananchi, na kujenga mwili, udugu na mshikamano katika jamii. Kwa hiyo:

**6.1.1.** **Vyombo vya habari yaani redio, magazeti, televisheni n.k. vitahimiza maadili, mila, desturi na utamaduni wetu.**

**6.1.2.** **Muda na vipindi vitakavyoonyeshwa na kutangazwa katika vituo vya redio na televisheni vitazingatia maadili, mila na desturi zetu. Aidha, vituo hivyo vitahimizwa kutoa nafasi zaidi kwa ajili ya muziki na sanaa za kitanzania.**

6.1.3. Maeneo ya wazi kwa ajili ya mapumziko na burudani kwa watoto na wazee yatatengwa na kusimamiwa kikamilifu.

6.1.4. Jamii, watu binafsi na mashirika mbalimbali yatahimizwa kujenga na kutunza maeneo kwa ajili ya burudani.

6.1.5. Vitawekwa vivutio kwa watengenezaji wa vifaa vyaburudani hapa nchini ili vifaa hivyo viweze kupatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu.

6.1.6. Serikali itahakikisha kwamba shughuli za burudani zitolewazo hazipotoshi maadili ya taifa.

6.1.7. Itahakikishwa kwamba utafiti kuhusu burudani za jadi unafanyika na kwamba matokeo ya utafiti huo yanasambazwa ili kurahisisha ufundishwaji na urithishwaji wa burudani za jadi.

6.1.8. Wanamichezo na wasanii watahamasishwa kutambua wajibu, haki na maslahi yao.

6.1.9. Itahakikishwa kuwa Majumba ya Maendeleo yaliyopo pote nchini yanatumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo na utoaji wa burudani, na pale ambapo hayapo, ujenzi wa nyumba za aina hii utahimizwa.

6.1.10. Asasi mbalimbali za Serikali, mashirika ya umma na ya watu binafsi na waajiri wengine, watatakiwa kutambua umuhimu wa burudani mahali pa kazi katika kuleta ufanisi wa utendaji na kuboresha afya ya wafanyakazi.

6.1.11. Michezo na sanaa zisizo za mashindano zitahimizwa na kuendelezwa katika jamii ili ziwe sehemu muhimu za burudani.

6.1.12. Wananchi watahamasishwa kutambua kuwa michezo ni muhimu katika kujenga mwili, afya, akili, nidhamu ushirikiano na uhusiano wa kimataifa.

6.1.13. Mipango ya uendelezaji wa ardhi na makazi itazingatia haja ya kujenga na kuwepo kwa maeneo ya michezo na burudani.

**6.1.14.** **Vitawekwa vivutio kwa watu binafsi na mashirika kuanzisha viwanda vya kutengeneza aina mbalimbali ya vifaa vya burudani humu nchini.**

## 7. UTAMADUNI NA USHIRIKISHWAJI UMMA

Kama ilivyokwisha kuelezwa, utamaduni ni matokeo ya mahusiano baina ya binadamu na mazingira yake. Katika rnsingi huu, utamaduni wowote ule hauwezi kuwa na thamani bila jamii inayohusika kushiriki na kushirikishwa kikamilifu katika kuutafiti, kuufufua, kuuhifadhi, kuuendeleza na kuuelezea. Kushiriki kwa jamii katika utamaduni wake huleta mshikamano na umoja, ubunifu, maendeleo na utambulisho wa jamii hiyo. Hivyo, Sera hii inalenga pia katika kuainisha namna jamii na vikundi mbalimbali vitakavyoshiriki na kushirikishwa katika kuuendeleza utamaduni.

### 7.1. Jamii na Utamaduni

Hapo awali jamii za kitanzania zilikuwa zikishiriki kikamilifu katika utamaduni wao. Lakini, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii baadhi ya wananchi wameanza ama kujiengua, au kuenguliwa na hivyo kutoshiriki kikamilifu katika utamaduni wao. Siku za karibuni kumezuka pia tabia ya baadhi ya watu wenye uwezo wa fedha kujiweka kati ya wananchi na mabingwa wa fani rnbalimbali za utamaduni. Watu hawa huwatumia mabingwa hawa kwa manufaa yao. Kutokana na hali hii, vikundi vingi na mabingwa hao wanakosa maslahi ambayo wangeyapata wao wenyewe binafsi na pia haki yao ya kuwasiliana moja kwa moja na umma. Hatma ya mwelekeo huu ni kudumaa kwa maendeleo ya wasanii na usanii, kupotoka kwa maadili na utamaduni wa taifa. Kuna haja ya jamii yenyewe pamoja na Serikali kushirikiana kikamilifu katika uendeshaji wa shughuli za utamaduni kwa kuzingatia misingi ya ushirikishwaji umma na demokrasia kwa manufaa ya taifa. Kwa hiyo:

**7.1.1. Kila mwananchi hana budi kutambua kuwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za utamaduni wake ni haki ya msingi.**

**7.1.2. Utaandaliwa utaratibu maalum utakaowawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za utamaduni.**

**7.1.3. Wananchi watahamasishwa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za utamaduni ikiwa ni pamoja na burudani na michezo.**

**7.1.4. Itahakikishwa kwamba vyombo vilivyokabidhiwa dhamana ya kusimamia na kuendeleza fani mbalimbali za utamaduni vinaendesha shughuli zake kwa uwazi na kwa kuzingatia sheria na demokrasia ili kuwapa fursa wananchi wengi kushiriki.**

**7.1.5. Wananchi watahamasishwa kuanzisha vyama vya fani mbalimbali za utamaduni.**

**7.1.6. Michezo kwa wote na matamasha vitahimizwa na kuendelezwa katika jamii.**

**7.1.7. Wananchi, makampuni na mashirika ya umma na ya watu binafsi watashirikishwa katika kuhakikisha kuwepo kwa maeneo, vifaa, mazingira na nyenzo mbalimbali za kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za utamaduni.**

**7.1.8. Utaandaliwa utaratibu utakaowawezesha watu wenye mahitaji maalum kama vile wazee na walemavu kushiriki katika shughuli mbalimbali za utamaduni.**

**7.1.9. Wananchi wataendelea kuwa huru kujipatia mapato kutokana na fani mbalimbali za utamaduni kulingana na sheria.**

## 8. MALEZI, ELIMU NA MAFUNZO

### 8.1 Malezi

Malezi ni elimu na mafunzo. Kumpatia mtoto malezi bora ni parnoja na kumpa elimu bora. Tangu zamani za kale malezi yalizingatia maadili, miiko, heshima, mila, desturi na itikadi ili kuwahusisha, kuwashirikisha na kuwawezesha watoto, vijana, watu wazima na wazee kutekeleza yale yanayotakiwa katika kuiendeleza jamii. Mkazo mkubwa wa malezi ni kurithisha mambo haya yote kwa vizazi vijavyo. Malezi yanayopendekezwa hapa ni yale yanayoanzia tangu mama anapotunga mimba, mtoto anapozaliwa na kukua hadi anapofikia umri wa miaka 18 anapotambuliwa kuwa ni mtu mzima. Mfumo na taratibu za jadi za kutoa malezi zimevurugika kutokana na mwingiliano wa mila na desturi za nchi na jamii mbalimbali, kupuuzwa na kudharauliwa kwa mambo ya jadi, mabadiliko ya kijamii na kiuchurni, na wazazi wenyewe kutotilia maanani malezi ya watoto wao. Aidha, baadhi ya wazazi wamekuwa wakitegernea kwamba jukumu la kulea lingetekelezwa na walimu shuleni, kwani watoto huanza shule mapema na huendelea kuwepo huko hadi wanapofikia umri mkubwa. Ili kuondokana na hali hii:

**8.1.1.** **Familia itatambuliwa kuwa ni asasi ya msingi na muhimu katika mfumo wetu wa jamii na itakuwa chimbuko na msingi wa kuendeleza maadili, elimu, mafunzo na utamaduni wetu.**

**8.1.2.** **Nafasi ya taasisi za dm1 katika kuendeleza maadili, elimu, mafunzo na utamaduni wetu itatambuliwa.**

**8.1.3.** **Mila na desturi nzuri zitatambuliwa, kuzingatiwa na kuendelezwa katika kujenga taifa lenye umoja, mshikamano, heshima, upendo na utulivu.**

**8.1.4.** **Kwa kuzingatia umuhimu wa wanawake katika malezi, elimu na mafunzo, nafasi ya wanawake katika kuendeleza malezi bora na urithishaji wa utamaduni katika jamii itazingatiwa katika mipango yote ya malezi, elimu na mafunzo.**

**8.1.5.** **Utafiti kuhusu malezi, mila, desturi na mazingira utahimizwa. Matokeo ya utafiti huo yatatumika katika kuboresha malezi, elimu na mafunzo.**

**8.1.6.** **Utaratibu wa kutunza, kuhifadhi na kuchapisha taarifa, takwimu na kumbukumbu za kiutamaduni utaanzishwa.**

**8.1.7.** **Jamii na wazazi watahimizwa kuenzi maadili, mila na desturi za malezi bora.**

**8.1.8.** **Serikali na jamii zitahakikisha kwamba haki za watoto zinalindwa.**

**8.1.9.** **Serikali itahakikisha kuwa watoto wenye umri wa kwenda shule wanakwenda shule na kwamba mitaala ya elimu na mafunzo itazingatia maadili ya kitanzania. Maadili haya ni pamoja na kuthamini utu, kuhimiza usawa wa kijinsia, kutunza mali na kuheshimu mila na desturi nzuri.**

**8.1.10.** **Taasisi zinazotoa elimu na mafunzo zitatambua na kutumia mila na desturi nzuri katika kuwaandaa vijana kuwa wazazi bora.**

**8.1.11.** **Mafunzo ya dini yatakuwa sehemu ya malezi ya watoto ili kusisitiza maadili, malezi mema, kazi, kustahiana na kuvumiliana.**

**8.1.12.** **Utawekwa utaratibu wa kuwawezesha watoto wa mitaani kupata malezi bora, elimu na stadi za kuwawezesha kuishi maisha ya heshima.**

**8.1.13.** **Wananchi watahimizwa kuzingatia kuwa uzalendo, kujali kazi, uadilifu, usafi, uhifadhi na utunzaji wa mazingira na rasilimali ni sehemu muhimu ya utamaduni wetu.**

### 8.2 Elimu na Mafunzo

Uendelezaji wa utamaduni unahitaji ujuzi na taaluma maalum kama vile, taaluma za michezo, fasihi, fasihi simulizi, makumbusho, elimu na makumbusho, maonyesho, palentolojia, akiolojia, uhifadhi nyaraka, uhifadhi majengo na maeneo ya mambo ya kale. utengenezaji wa maleba, mbinu za utafiti, ngoma na kadhalika. Mengi ya masomo haya na taaluma

zinazohusika hazifundishwi katika chuo chochote hapa nchini. Ndiyo maana Sekta ya Utamaduni ina wataalam wachache katika fani hizo. Wengi wa wataalam waliopo katika Sekta hii wamepata mafunzo yao nje ya nchi. Kutokana na hali hii, maafisa wengi wanaosimamia shughuli za utamaduni hasa katika ngazi ya mkoa na wilaya hawana taaluma, mafunzo na elimu ya kutosha katika maeneo wanayoyashughulikia. Kwa hiyo:

**8.2.1. Serikali itahimiza uanzishaji wa vyuo na taasisi mahususi za kufundisha fani mbalimbali za utamaduni.**

**8.2.2. Ufundi wa jadi pamoja na mfumo wa mafunzo ya ufundi wa jadi vitatambuliwa na kuendelezwa kuwa sehemu ya elimu na mafunzo stadi.**

**8.2.3. Serikali itahimiza ufundishaji wa taaluma za makumbusho, mambo ya kale, nyaraka na ukutubi katika ngazi za elimu na mafunzo ya juu.**

**8.2.4. Serikali itaimarisha shule na vyuo vyake vya fani za michezo, ukutubi, utunzaji nyaraka na sanaa, na kuanzisha chuo cha mafunzo kuhusu uhifadhi wa majengo na maeneo ya kale.**

**8.2.5. Mitaala ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu itajumuisha mafunzo kuhusu sanaa za aina mbalimbali kwa mfano, muziki, uchoraji, uchongaji na tamthiliya. Aidha, masomo haya yatatahiniwa katika mitihani ya mwisho ya ngazi hizi za elimu.**

**8.2.6. Aina zote za elimu zitatambua na kuhimiza matumizi ya makumbusho, mambo ya kale, maktaba na nyaraka kama vielelezo katika utoaji wa elimu na mafunzo nchini.**

**8.2.7. Stadi za kusoma, kuhesabu na kuandika zitatambuliwa kuwa ni sehemu ya utamaduni wetu na hivyo kuhimizwa.**

**8.2.8. Watu binafsi na mashirika mbalimbali wataruhusiwa kuanzisha, kumiliki na kuendesha taasisi za elimu na mafunzo katika fani mbalimbali za utamaduni. Aidha, zitawekwa sheria zitakazoongoza uanzishwaji na uendeshaji wa taasisi hizo.**

**8.2.9.** **Watendaji katika Sekta ya Utamaduni watatakiwa kujiendeleza katika taaluma na fani zao iii kuongeza tija na ufanisi kazini.**

**8.2.10.** **Wananchi watahimizwa kujiwekea malengo katika maisha yao, kuzingatia dhana ya ushindani na utumiaji wa nyenzo za kisasa katika uzalishaji mali kupima tija na kuweka kumbukumbu za shughuli zao za kila siku.**

## 9. UJENDESHAJI NA UGHARIMIAJI WA SHUGHULI ZA UTAMADUNI

### 9.1 Uendeshaji

Shughuli za utarnaduni huendeshwa, kwa kiasi kikubwa, na wananchi wenyewe. Jukumu la Serikali ni kuweka sera, kuratibu na kusimamia uendeshaji wa shughuli hizi, hususan katika ngazi ya taifa, mikoa na wilaya. Ufanisi, uendeshaji na usimamizi wa shughuli za utamaduni unategemea sana ubora wa watendaji, taaluma walizonazo watendaji hawa, muundo, rntiririko na mgawanyo wa madaraka uliopo, nyenzo za kufanyia kazi, na uzito ambao Serikali itatoa kwa Sekta hii. Hivi sasa, katika ngazi ya taifa, Sekta hii inaongozwa na Kamishna wa Utarnaduni, akisaidiwa na Wakurugenzi wa Idara za Nyaraka za Taifa, Sanaa na Lugha, Mambo ya Kale na Maendeleo ya Michezo. Uhifadhi wa Mambo ya Kale na Nyaraka za Taifa unaendeshwa chini ya Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na Sheria ya Nyaraka za Taifa ya 1965. Pamoja na Idara hizi kuna Shirika la Makumbusho ya Taifa ambalo liliundwa kwa Sheria ya Makumbusho ya Taifa ya mwaka 1962; Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) lililoundwa kwa Sheria ya Baraza Ia Sanaa la Taifa ya mwaka 1984; Bodi ya Filamu na Michezo ya Jukwaani iliyoundwa kwa Sheria ya jina hilo hilo ya rnwaka 1976; Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) Iililoundwa kwa Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa ya mwaka 1967 na Baraza Ta Michezo la Taifa (BMT) lililoundwa kwa Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ya mwaka 1967. Baadhi ya sheria zilizotajwa hapo juu zilirekebishwa au kuhuishwa kati ya mwaka 1970 na 1985 kama inavyoonyeshwa katika mabano: Sheria ya Mambo ya Kale (1979, 1991); Sheria ya Nyaraka za Taifa, Sheria ya Makumbusho ya Taifa (1980); Baraza Ia Kiswahili la Taifa (1983); Baraza la Michezo Ia Taifa (1971) na Sheria ya Baraza Ta Sanaa Ia Taifa (1984). Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, inabidi sheria hizi ziangaliwe upya.

Idadi ya watumishi waliopo katika ngazi ya mkoa na wilaya hailingani na majukurnu yanayotakiwa kutekelezwa katika ngazi hizo. Katika baadhi ya mikoa na wilaya, hakuna watumishi wanaotarajiwa kuwepo au kama wapo, hawatoshi. Kwa rnfano, Halmashauri nyingi za Wilaya na Miji hazina ikama ya Maafisa Utamaduni. Hali hii imesababisha dhima ya utamaduni kuendelea kutokutambuliwa, kutokueleweka, kutokuthaminiwa na kutokutumiwa kikarnilifu katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Katika ngazi ya mkoa na wilaya, Sekta ya Utarnaduni huongozwa na Afisa Utamaduni ambaye anatakiwa kuwa na wasaidizi ambao ni wataalam katika maendeleo ya michezo, sanaa na lugha. Katika ngazi ya wilaya, Sekta ya Utamaduni ipo chini ya Idara ya Elimu kutokana na muundo wa Serikali za Mitaa. Idara za Mambo ya Kale na Nyaraka za Taifa hazikuwa na watumishi katika ngazi ya mkoa na wilaya, kwani, Idara hizi zimekuwa zikitegemewa kuendesha kazi zake kutoka makao makuu ya Idara yaliyopo Dar es Salaam.

Kwa kutambua kwamba utamaduni ni msingi na dira ya maendeleo ya taifa lolote lile, Serikali inaona umuhimu wa kuimarisha na kuboresha uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Sekta ya Utamaduni. Kwa hiyo:

**9.1.1.** **Sekta ya Utamaduni, itaendelea kuwa na nafasi katika Mfumo wa Serikali.**

**9.1.2.** **Serikali itaandaa na itasimamia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni na itahuisha sheria zinazohusiana na shughuli za utamaduni.**

**9.1.3.** **Asasi zinazoshughulikia masuala na fani za utamaduni zitaimarishwa kwa kuzipatia nyenzo na vitendea kazi vya kutosha pamoja na wataalam wenye sifa na ujuzi unaostahili.**

**9.1.4.** **Patakuwepo na maafisa watakaoshughulikia masuala ya utamaduni katika ngazi ya mkoa na wilaya. Maafisa hawa watasaidiwa na wataalam wa Michezo, Sanaa, Lugha, Nyaraka na Mambo ya Kale.**

**9.1.5.** **Waendeshaji wakuu wa shughuli za utamaduni katika ngazi za taifa, mikoa na wilaya, watatakiwa kuwa na shahada ya chuo kikuu, utaalam katika mojawapo ya fani za utamaduni, mafunzo ya utawala na uendeshaji pamoja na uzoefu wa kazi.**

**9.1.6.** **Waendeshaji wakuu wa shughuli za utamaduni katika ngazi ya taifa, mikoa na wilaya watakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya utamaduni na shughuli za utamaduni katika maeneo yao.**

**9.1.7.** **Wakuu wa vyuo na taasisi zinazotoa elimu na mafunzo katika fani za utamaduni watatakiwa kuwa na angalau shahada ya uzamili katika mojawapo ya fani za utamaduni.**

**9.1.8.** **Wasimamizi na watendaji wakuu wa shughuli za utamaduni katika ngazi za taifa, mkoa, wilaya na taasisi za elimu na mafunzo watapata mafunzo ya uendeshaji na usimamizi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.**

**9.1.9.** **Wizara yenye dhamana ya utamaduni itaweka utaratibu maalum wa kusajili na kusimamia mafunzo ya fani za utamaduni zinazoweza kuhatarisha usalama wa raia na mali kama vile mieleka, mazingaombwe, Kung Fu, ngumi, karate na judo.**

**9.1.10.** **Serikali itaanzisha taratibu zitakazowezesha usajili wa shule, vyuo na wataalam wa fani mbalimbali za utamaduni ili kuzuia kushuka kwa viwango vya taaluma na ukiukwaji wa taratibu.**

**9.1.11.** **Shirika la Makumbusho ya Taifa, BASATA, BAKITA, BMT na Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Sanaa za Maonyesho yatahimiza na kutoa ushauri kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa asasi za aina hiyo katika ngazi za mikoa, wilaya hadi vijijini.**

**9.1.12.** **Sheria zilizopo zitatafsiriwa na kuchapishwa katika lugha ya Kiswahili ili wananchi walio wengi waweze kuzisoma na kuzielewa.**

**9.1.13.** **Wananchi watahimizwa kuzielewa na kuziheshimu sheria na kanuni zilizowekwa na kutambua kwamba ni wajibu wa kila mwananchi kutii sheria.**

**9.1.14.** **Adhabu kali zaidi zitatolewa kwa wanaotiwa hatiani kwa kukiuka sheria na kanuni zinazolinda maadili ya taifa.**

**9.2 Maadili ya Utambulisho wa Taifa**

Lazima tuwe na taratibu maalum ambazo zitalinda hadhi ya utambulisho wetu. Ili kutekeleza azma hii:

**9.2.1.** **Vitambulisho vya Taifa kama vile Mlima Kilimanjaro; Twiga; Bendera ya Taifa; Wimbo wa Taifa, Mwenge wa Uhuru; Nembo ya Serikali na kadhalika vitabainishwa kisheria ili wananchi wavitambue, waviheshimu na kuvilinda ipasavyo.**

**9.2.2.** **Misingi ya Katiba ya Taifa itafundishwa kwa wanafunzi wote katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari. Mafunzo haya yatakuwa ni pamoja na majukumu na wajibu wa raia.**

**9.2.3.** **Wimbo wa Taifa utafundishwa kwa wanafunzi wote kuanzia shule za awali.**

**9.2.4.** **Katika shule za awali, msingi na sekondari Wimbo wa Taifa utaimbwa kila siku kabla wanafunzi hawajaingia darasani.**

**9.2.5.** **Watu wote watasimama na kuimba Wimbo wa Taifa kabla ya kuanza maonyesho na michezo yote yenye hadhi ya kitaifa na kimataifa.**

**9.2.6.** **Itakuwa marufuku kupandisha Bendera ya Taifa iliyopasuka au kupauka. Aidha, Serikali itaandaa taratibu na kuziweka wazi kuhusu ni lini na wapi Bendera ya Taifa inaweza kupandishwa au kutumiwa.**

**9.2.7.** **Mwenge wa Uhuru utaendelea kukimbizwa nchini na Serikali itahakikisha kwamba wananchi wote wanauthamini.**

**9.2.8.** **Wananchi watashirikishwa katika kubuni na kuchagua majina ya maeneo na nembo za wilaya, mikoa na taifa. Maumbile, uoto na viumbe asilia vitafikiriwa wakati wa kubuni nembo mpya. Nembo ambazo tayari zinatumiwa zitawekwa wazi ili wananchi wazifahamu na kuzipatia hadhi inayostahili.**

**9.2.9.** **Zitabuniwa nyimbo maalum ambazo zitafundishwa kwa wanafunzi na wananchi kwa jumla ili ziwe sehemu ya utambulisho wao.**

**9.2.10.** **Yatakuwepo mavazi maalum ambayo yatakuwa sehemu ya Utambulisho wa Taifa.**

### 9.3 Hakimiliki

Maslahi na haki za wasanii, watunzi, waandishi, wachapishaji, wabunifu na wengine wote wanaotoa mchango wao katika kukuza na kuendeleza utamaduni lazima yaheshimiwe na kulindwa kulingana na sheria za hakimiliki za kitaifa na za kimataifa. Jamii inawajibika kuhakikisha kuwa kila rntu anapata malipo kamili na halali kutokana na juhudi zake. Kwa hiyo:

**9.3.1.** **Serikali itaanzisha chombo cha kusimamia Hakimiliki.**

**9.3.2.** **Tanzania itaridhia mikataba na kujiunga na asasi muhimu za Hakirniliki za Kimataifa karna vile, 'Berne Convention' na 'Universal Copyright Convention'.**

**9.3.3.** **Utekelezaji na uhuishaji wa sheria zinazohusu Hakimiliki utahirnizwa ili sheria hizi ziendane na wakati na mabadiliko ya teknolojia.**

### 9.4 Maendeleo ya Wananchi na Utamaduni

Serikali inatambua kwamba wajibu wa kuendeleza utamaduni siyo wake peke yake na hivyo ni lazima wananchi washirikishwe katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli hizi. Kwa hiyo:

**9.4.1.** **Wananchi watahamasishwa kutambua kwamba wanao wajibu mkubwa wa kulinda na kuhifadhi urithi wetu wa utamaduni, maumbile ya asilia na mazingira katika miji, vijiji na maeneo yao.**

**9.4.2.** **Wananchi watahimizwa kuwatambua watu wenye uwezo na vipaji maalum vinavyohusu utamaduni miongoni mwao na kuwaenzi inavyopasa.**

**9.4.3.** **Watu wenye vipaji maalum vinavyohusu utamaduni hawana budi wajitambue, wajiamini na watumie vipaji vyao kujiendeleza, kujikimu, kuuelimisha umma na kuendeleza maadili.**

**9.4.4.** **Watu wenye ujuzi katika fani za kiutamaduni ambazo zinaweza zikahatarisha usalama wa raia na mali watatambuliwa na kuwekewa taratibu maalum za kudhibiti matumizi ya ujuzi wao. Fani hizo ni kama vile mieleka, mazingaombwe, judo, ngumi, karate na Kung Fu.**

**9.4.5.** **Watu wenye ujuzi na vipaji maalum watahimizwa kurithisha taaluma na ujuzi walionao.**

**9.4.6.** **Kamati za Elimu na Utamaduni za Mamlaka za Serikali za Mitaa zitahamasishwa kuratibu na kusimamia uendeshaji wa shughuli za utamaduni, kama vile, kutenga na kulinda maeneo ya burudani, michezo na urithi wa utamaduni, na kujenga na kuendesha Makumbusho na Nyumba za Maendeleo.**

## 9.5 Ugharimiaji

Ugharimiaji wa shughuli za utamaduni ni jukumu Ia wananchi wenyewe, watumiaji wa huduma hizo na Serikali. Hata hivyo, imedhihirika kwamba tangu wakati wa ukoloni wananchi wamekuwa wakitegemea kwamba Serikali peke yake ndiyo yenye jukumu la kugharimia shughuli za utamaduni. Hali hii imekithiri katika kushiriki kwa timu na vikundi vya michezo na sanaa kwenye mashindano na maonyesho ya ngazi zote. Hivi sasa shughuli za Serikali zimepanuka na gharama za uendeshaji zimeongezeka kiasi kwamba Serikali haiwezi kuendelea kuubeha mzigo huu peke yake. Vile vile, Serikali peke yake ndiyo ambayo imekuwa inabeba mzigo wa kugharimia shughuli na nyaraka, mambo ya kale na makumbusho. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuangalia upya mfumo uliopo wa kugharimia shughuli za utamaduni ili kuwahusisha wananchi na watumiaji wengine na hivyo kupanua vyanzo vya mapato ya kugharimia uendeshaji wa shughuli hizi. Katika kutekeleza azma hii:

**9.5.1.** **Serikali itawahamasisha na kuwashirikisha watu binafsi, mashirika mbalimbali na jamii kwa jumla kuchangia na kugharimia uendeshaji wa shughuli za utamaduni.**

**9.5.2.** **Vikundi, Vilabu, Vyama na Mabaraza mbalimbali ya fani za utamaduni yatahimizwa kujiendesha na kujitegemea.**

**9.5.3.** **Taasisi na vyuo vinavyotoa elimu na mafunzo ya fani mbalimbali za utamaduni vitatoza karo. Karo hizo zitatumika katika uendeshaji wa taasisi au vyuo hivyo.**

**9.5.4.** **Asasi zinazotoa huduma za utamaduni zitatoza ada. Ada hizo zitatumika katika kuendeleza fani husika.**

**9.5.5.** **Serikali itatoza kodi ya burudani ili kugharimia uendeshaji wa shughuli za utamaduni.**

**9.5.6.** **Taasisi na vyuo vinavyotoa elimu na mafunzo ya fani za utamaduni vitahimizwa kuwa na shughuli za kujiongezea mapato.**

**9.5.7.** **Huduma na bidhaa zitakazotengenezwa na kutolewa na asasi za utamaduni zitauzwa kibiashara.**

**9.5.8.** **Watu binafsi na mashirika mbalimbali yatahimizwa kuwekeza rasilimali katika Sekta ya Utamaduni.**

### 9.6. Mgawanyo wa Majukumu

Ingawaje majukumu ya Serikali na Sekta Binafsi yameainishwa katika Sera hii kuna umuhimu wa kuweka wazi majukumu ya jumia ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi. Majukumu hayo ni haya yafuatayo:

**SERIKALI KUU**

**9.6.1. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni.**

**9.6.2. Kuweka mfumo na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa utamaduni.**

**9.6.3. Kuandaa mitaala na kusimamia mafunzo ya taaluma zinazohusu fani mbalimbali na utamaduni.**

**9.6.4. Kuweka vivutio na kuihimiza sekta binafsi ili iweze kuwekeza rasilimali katika Sekta ya Utamaduni ikiwa ni pamoja na viwanja vya michezo na burudani, kumbi za maonyesho, makumbusho za aina mbalimbali, maktaba, viwanda vya kutengenezea vifaa 'vya michezo, sanaa na tasnia nyingine za utamaduni.**

**9.6.5. Kuhimiza Wizara, Mashirika na Taasisi za Umma kuthamini na kutumia fani mbalimbali za utamaduni kwa ajili ya burudani na kuchochea uzalishaji mali.**

**9.6.6. Kugharimia uendeshaji wa shughuli za utamaduni katika ngazi ya taifa na kimataifa.**

**9.6.7. Kuhakikisha kwamba tathmini ya athari za miradi mbalimbali ya maendeleo kwa utamaduni wetu inafanyika kabla ya kutekelezwa kwa miradi hiyo.**

**9.6.8. Kuanzisha Mifuko na kodi maalum kwa ajili ya kugharimia uhifadhi na uendelezaji wa utamaduni.**

**SERIKALI ZA MITAA**

**9.6.9. Kugharimia uendeshaji wa shughuli mbalimbali za utamaduni katika ngazi ya Wilaya.**

**9.6.10. Kuweka Sekta ya Utamaduni katika mfumo wa uendeshaji wa Serikali za Mitaa.**

**9.6.11. Kuhamasisha wananchi kujivunia, kushiriki na kuhifadhi utamaduni wao.**

**9.6.12. Kutumia fani mbalimbali za utamaduni kama kichocheo cha maendeleo ya jamii na kiuchumi.**

**9.6.13. Kuziona na kuzitambua fani mbalimbali za utamaduni kuwa ni vyanzo vya mapato na maeneo ya uwekezaji.**

**SEKTA BINAFSI**

**9.6.14. Kushirkiana kikamilifu na Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni.**

**9.6.15. Kuziona na kuzitambua fani mbalimbali za utamaduni kuwa ni mojawapo ya maeneo muhimu ya uwekezaji.**

**9.6.16. Kuandaa na kuendesha mashindano na maonyesho ya michezo, sanaa, burudani na tasnia za utamaduni.**

WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI